Pasteur Kitoka Moke Mutondo

SOMO KWA WAFUASI WA SHULE LA UBATIZO

Kitabu cha Mwalimu

YALIYOMO

KIINGILIO……..……...3
I. MWITO……...……..……..4
II. IMANI YA WAKRISTO.....6
2.1. Imani kuhusu Biblia 6
2.2. Imani kuhusu Mungu.....7
2.3. Imani kuhusu uhumbaji 8
2.4. Imani kuhusu Malaika 8
2.5. Imani kuhusu zambi 8
2.6. Imani kuhusu Wokovu 9
2.7. Imani kuhusu Kanisa 9
2.8. Imani kuhusu Sakramenta 9
2.9. Imani kuhusu siku za mwisho 10
III. NJIA ZA KUKOMAA KIROHO……..……11
3.1. Kufuata mafundisho.....11
3.2. Kufuata Mahubiri.....11
3.3. Kusoma neno la Mungu kila siku 12
3.4. Kua na mda binafsi wa maombi.....12
3.5. Kuomba mashauri 12
3.6. Kushirikiana na wakristo wengine.....13
KWA MWISHO…….……**13**

KIINGILIO

Wakati mtu anamwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake, anakuwa kiumbe kipya ao amezaliwa mara ya pili. Ime mpasa kubatizwa kwa maji mengi ili apate kuwa mwanamemba wa kanisa la mahali (2 Wakorinto 5 :17).

Kwa hivi, yeye ni kiungo katika mwili wa Kristo ambalo ni Kanisa. Kwa mkristo mpya kuwa kiungo kinachofaa kwa Mungu na kwa kanisa lake, nilazima afahamu mambo tatu yatakayo msaidia katika safari yake ya kwenda mbingu : Habari za mwito, Imani ya wakristo na kanuni za kukomaa kiroho.

Kwa siku hizi za mwisho ambako walimu wa uwongo ni wengi, ni lazima kwa walimu wa shule la ubatizo wawe na kitabu kitakacho waongoza katika mafundisho ya wakristo wapya na wazamani ambao wanawajibika kuelewa msingi wa imani yao katika Kristo.

Tunatoa shukrani zetu kwa wachungaji Yoheli BYALUNGWA, SHINDANO MASILYA na BALIWA walioleta mawazo ya kuandika kitabu hiki kwa ajili ya walimu wa shule la ubatizo. Maonyi, mashauri na mafazaiko yao ilitusaidia kufikia hapa.

Utajiri wa kitabu hiki ni kwamba mafundisho yaliyomo yanawezwa kueleweka na watoto wa miaka 12 na watu wakubwa ambao wote ni wachanga kiroho. Ndio sababu, mwalimu wa shule la ubatizo anaitajika kuwa mtu wa maombi, mwenye kuelewa Maandiko matakatifu, wa juhudi na mvumilivu akifahamu ya kwamba ni Roho Mtakatifu ndie atamsaidia kutafsiri mafundisho yake kwa kila mwanafunzi.

Kitabu hiki hakikomboe Biblia ambayo ni msingi wa Imani ya wakristo. Kwa hivi, mwalimu wa shule la ubatizo ana hitajika kuongeza shahiri zingine za Biblia, mafundisho mengine kuhusu Imani, Maombi, maisha ya utakaso, utowaji, mapashwa ya mkristo mbele ya kanisa lake, na kazalika.
Pamoja na mafundisho, ni lazima mwalimu wa shule la ubatizo awe na mda wa maombi na wanafunzi wake kusudi awazoeze maisha ya maombi.

Katika kuandika kitabu hiki tulitumia pia kitabu cha Doctrine, discipline et liturgie ya 8ème CEPAC iliokubaliwa na assemblée général ya mwezi wa nane 2007.

I. MWITO

Mwito ni aliko mwanadamu anapokea toka Mungu ili amtumikie. Kwa hivi mwito ni neno la kwanza na la lazima katika maisha ya ukristo. Ni vigumu kwa mwanadamu kuwa mkristo anayefaa mbele za Mungu na Kanisa ikiwa yeye hakuitwa na Mungu binafsi.

Katika Biblia tunakuta watu wengi walio itwa na Mungu kwa kazi yake : Ibrahmu (Mwanzo 12 :1), Musa (Kutoka 3 :1-13), Samweli (1 Samueli 3 :3-7), Petro na Andrea (Matthieu 4 : 18-19).
Kupitia mifano haya, mwalimu ataonyesha wafuasi kwamba, Mungu anamwona mwanadamu popote alipo na anaita watu kila siku ili wamuamini na wamtumikie (Ufunuo 3 :20). Kwa hivi, ni lazima wanadamu wawe tayari na kufahamu kwamba siku ya mwanadamu kuitwa na Mungu inaweza fika kila wakati.

Ni lazima kwa mwalimu kukanusha mafundisho ya uongo (ya prédestination) inayofundisha ya kwamba si watu wote ndio wataitwa (kuokolewa) na Mungu, bali ni wale tu walio tayarishwa na Mungu tangu zamani (prédestination). Mafundisho haya ni ya uwongo sababu Biblia inafundisha ya kwamba kila amuamie Yesu ataokolea (Kumbukumbu la Torati 10 : 17, Yohana 3 :16 ; Marko 16 : 16 ; Matendo 10 : 34 ; 16 : 31). Mahandiko haya na mengine yanaonyesha Kwamba Mungu hana upendeleo na kila mwanadamu anaye muamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wa Maisha yake, ataokolewa.

Sababu hii, ni lazima kwa kila mwanadamu anaye mwamini Kristo na kubatizwa awe na uhakika wa mwito wake. Kwa hivi, kila mkristo mpya anapashwa kujiuliza maulizo tatu kuhusu mwito wake katika maisha ya ukristo.

1.1. Nani aliniita kuwa mkristo ?

Magonvi na makelele mingi yanayo tesa kanisa leo yanatokana na namna mbalimbali ambazo watu wengi wanaingia katika kanisa. Katikati ya wale wanao batizwa, kuna walio itwa na jamaa zao, walio itwa na marafiki zao, walio itwa na tamaa yao, walio itwa na kabila lao ao walio itwa kwa kufuata faida fulani ; na kuna wale walio itwa na Mungu mwenyewe.

Kwa mwanadamu kuwa mkristo anayefalia Mungu na Kanisa ni lazima ahakikishe kwamba aliitwa na Mungu peke yake na ya kwamba kazi zote anazo zifanya anazifanya kwa kumupendeza Mungu aliye muita (1 Wakorinto 10 : 31).

Pasipo kuitwa na Mungu inamufanya yule aliyebatizwa kuwa mutu wa uvuguvugu na mwenye kukwaza wengine katika Kanisa sababu anatumikia wanadamu na umoja na maendeleo ya kanisa sio shuguli lake.

Ulizo hili liliwasaidia sana Musa na Mtume Paulo kufaulu katika utumishi wao. Ndio sababu Mtume Paulo alianza kuandika barua zake katika kuonyesha ni nani alimwita kua Mtume: *Paulo, Mutume (si wa watu, wala kwa mutu, ila kwa Yesu Kristo na Mungu Baba aliye mufufua toka wafu)* (1 Wakorinto 1 :1).

Kufahamu nani alimuita kutamusaidia mkristo mpya kuwa kiumbe kipya kinacho mupendeza Mungu na kushiriki katika maendeleo ya kanisa lake. Sababu walijua ni nani aliwaita, Musa na Paulo walipata jibu kwa matatizo walio kutana katika utumishiwao:

- Wakati alipata shida ya kuvusha wana wa Israeli bahari nyekundu, aliposhambuliwa na ndugu zake kwa kukosa chakula, taifa lingine lilipokuja kumupiganisha, Musa hakulalamika wala kuomba msaada kwa ndugu zake wala hakumwita baba mkwe wake Yetero amutetee; lakini alimukimbilia Mungu peke yake, sababu alifahamu kwamba si ndugu zake wala Yetero ndio walimuita akombowe wa Israeli (Kutoka 14:10-14; 15:22-27; 16:1-11).
- Paulo na Sila walipo tupwa gerezani baada ya kupigwa uchi sokoni, Paulo hakutuma watu wamwite Anania aliye muwekea mikono aje awatetee; lakini, usiku wote walikesha wakimwimbia na kumuabudu Mungu aliye waita (Matendo 15:22-40)

- Katika utumishi wao, Musa na Paulo walitafuta kumpendeza Mungu, kuliko kupendeza wanadamu ambao hawakuwafanya kuwa watumishi.

- Katika utumishi wao Musa na Paulo walitafuta tu sifa na faida ya Mungu aliye waita, sio sifa wala faida yao wenyewe ao ya jamaa zao.

Ni lazima kila mkristo mpya aelewe ya kwamba katika maisha mapya anayo yaanza, kuna majaribu na matatizo mengi, bila kuitwa na Mungu na kumutegemea hawezi kushinda.

1.2. Namna gani niliitwa?

Ni muhimu sana kwa kila mkristo mpya kuelewa namna gani aliitwa.

Wakati Mtume Paulo anapo jitaja kuwa Mtumishi *kwa mapenzi ya Mungu* (1 Kor.1:1a) anapenda kuonyesha ya kwamba yeye ni Mutumishi *kwa neema ya Mungu*, wala si kwa sababu ya kufunzwa na Gamalieli ao sababu yeye ni muyuda.

Mara nyingi wakristo wapya ujaa kiburi na kufikiri ya kwamba ni kwa sababu ya mali yao, ya kabila zao ao masomo yao ndio wao ni wa kristo leo. Hali hii inatuma wengi wao wanakosa unyenyekevu na kuwaka kiburi wakifikiri wao ni wa lazima kuliko wengine na bila wao kanisa haliweze kuendelea. Kwa hivi, unyenyekevu ni wa lazima katika maisha mapya ya ukristo.

Picha ya Kanisa inayo fananishwa na mwili, inapenda kuonyesha ya kwamba katika Kanisa hakuna mkristo ao huduma ilio ya lazima kuliko zingine; ila kila mmoja analazima ya mwengine kwa kukomaa na kuendelea katika maisha inayo mupendeza Mungu.

Ni lazima kwa kila mkristo mpya kuelewa ya kwamba anapashwa kutumikia Mungu katika unyenyekevu akishirikiana na wakristo wengine kwa kuendelesha kazi ya Bwana.

Neno hili lilimusaidia pia Paulo kuwa kiongozi mutumishi pahali pa kuwa kiongozi mukubwa mbele ya wengine wote (Waroma 12:3 ; 1Wakorinto 4:7; 15:10-11).

1.2. Niliitwa kufanya kazi gani?

Ulizo la tatu kila mkristo mpya anapashwa kujiuliza kuusu mwito wake ni la kujuwa huduma gani aliitwa kufanya katika Kanisa. Haiwezekane kwa mkristo mpya kuwa katika kanisa na kufikiri yeye hana

kazi ao huduma ya kufanya; bali ni Muchungaji, Wazee, Wainjilisti, mashemasi ao waimbaji tu ndio wanakazi ya kufanya kanisani. Wazo kama na hili halina nafasi katika kanisa ulio mwili wa Kristo!

Haiwezekane Mukristo mpya afae kwa Kanisa lake kabla haja elewa karama gani anakuwa nayo na kwa njia gani anaweza kuitumikisha na kushiriki katika maendeleo ya mwili wa Kristo. Hii itamsaidia kuhepuka uvuguvugu, kuparamia huduma na kusikia wivu ya wengine kwa huduma wanazo zifanya kanisani.

Mtume Paulo, japokuwa ni yeye alianzisha makanisa katika Azia, hakujifanya Mchungaji wa kanisa la fasi, wala hakuhusika na kugawa chakula na misaada mbalimbali ; sababu alijua kwamba Mungu alimuita li atangaze habari njema (Evangéliste) peke yake na huduma zingine zitafanywa na wakristo wenye kua na karama hizo (Waroma 1:1c).
Ni lazima kila mkristo mpya awe na muda wa maombi na kuuliza Bwana ampe karama itakayo mupatia huduma katika kanisa; sababu ni karama ndio inamupa mukristo huduma kanisani.

II. IMANI YA WAKRISTO

Mbele ya mwamini mpya kubatizwa, ni muhimu afundishwe imani mpya ili achague mwenyewe ikiwa amekubali kuifuata ao hapana. Ndio sababu, zehebu la 8ème CEPAC halibatize watoto wadogo ila tu watu walio na umri wa miaka 12 inayojulikana kuwa umri wa mtu kufikiri[1]. Hatua hii ilichukuliwa kufuatana na andiko la Marko 16: 16 linalofundisha kwamba *ni yule anaye amini ndie atabatizwa*.

Ni lazima kwa mwamini mpya kufahamu nini Mungu anataka aamini na afanye.
Japokua tumefanya hivi, mwalimu ataanza kwanza kutayarisha somo lake na majibu kwa maulizo. Kwa mfano, siku mwalimu atafundisha kuhusu elimu ya Biblia, ni lazima awe tayari kutaja vitabu vyote 66 vya Biblia bila kusoma na atachukuwa majibu ya maulizo kuhusu Biblia na kuyatayarisha kama somo la kufundisha mbele ya kuuliza maulizo yaliyo ndani ya somo kwa wafuasi.

2.1. Imani kuhusu Biblia

Mbele ya kuanza somo lake, mwalimu wa shule la ubatizo ata shurutisha kila mfuasi awe na Biblia yake kila siku ya shule.

Katika zehzbu la 8ème CEPAC, tumeamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililo andikwa kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu ili litufunulie Mungu ni nani na ni nini iliyo mapenzi yake.
Kwa hiyo, ni Biblia peke yake ndio Kitabu kinachoweza kutusaidia kufahamu yale Mungu anataka tuamini na tufanye.

Biblia ina sehemu mbili: Agano la Kale lililo na vitabu 39 na Agano Jipya lililo na vitabu 27[2].
Agano Jipya ni utimilifu wa Agano la Kale, ni ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo na ni Neno la Mungu (Matayo 5 : 18 ; Luka 24 : 44 ; Yohana 10 :35 ; 1 Wakorinto 15 : 3-4 ; Wakolosayi 1 : 16 ; 2 Timotéo 3 : 15-17 ; 1 Petro 1 : 10-12 ; 2 Petro1 : 20-21 ; 3 : 15-16).

[1] âge de raison
[2] Mwalimu atataja vitabu vyote vya Biblia na kumuomba kila mfuasi avitaje kwa ufahamu bila kuangalia katika Biblia yake

Maulizo :

- Wapi tunaweza kuvumbua Mungu ni nani na nini iliyo mapenzi yake ?
- Biblia ni nini ?
- Taja na ufasiriye mgawanyiko wa Biblia.

2.2. Imani kuhusu Mungu

Biblia inatufundisha ya kwamba Mungu ni Baba yetu anayekaa mbinguni, ni yeye aliye umba vitu vyote na anayeongoza vitu vyote katika hekima, haki na upendo.

Katika zehebu la 8ème CEPAC, tunaamini ya kwamba kuna Mungu mmoja tu ambaye hana mwanzo wala mwisho, yeye ni Milele, hana mipaka, anaona mahali pote, anauwezo na najuwa mambo yote (Mwanzo 1 :1 ; Kutoka 3 : 14 ; Kumbukumbu la Torati 6 :4 ; Psaumes 139 : 7-12 ; 24 :4 ; Mezali 15 : 3 ; Matayo 28 : 19 ; Yohana 5 : 58 ; Waebrania 1 : 2-3).
Mungu ananafsi tatu : Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu.

Mungu ni Roho na nilazima wanao muabudu wamuabudu katika roho na kweli.
Biblia inafundisha ya kwamba Mungu anaitaji tumpende kwa moyo wetu wote, kwa nguvu zetu zote na kwa mafikiri yetu yote na tuwapende watu wengine kama tunavyojipenda wenyewe.

Mungu Baba ni muumbaji wa vitu vyote vilivyo mbinguni na Duniani. Yeye ni mwanzo na mwisho. Pamoja na Mungu mwana na Mungu Roho Mtakatifu, aliumba mtu kwa mfano wake.

Biblia inafundisha ya kwamba Yesu Kristo ni Mungu kweli na mtu kwali aliye chukua mwili wa binadamu. Alizaliwa na bikira Maria kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Matayo 1 :20-25 ; 16 :15-16 ; Luka 1 : 26-35 ; Yohana 1 : 1-18 ; Matendo 2 :22-36 ; Waroma 8 : 3, 32-34 ; Wagalatia 4 : 4-5 ; Wafilipi 2 :5-11 ; Wakolosayi 1 : 12-22 ; 1 Timoteo 6 : 14-16 ; Waebrania 1 : 1-5 ; 1 Yahana 1 : 1-3 ; 4 :2-5).

Roho Mtakatifu ni Mungu na ni yeye ndie alivuvia wandishi wa Biblia. Ni yeye anaye hakikishia watu zambi zao na kuwavuta wazitubu na kuzikiri, anabatiza, anatakasa, anakaa ndani ya wakristo, anafariji, anakumbusha, anatia nguvu, anaongoza katika maisha ya utakaso, anashuhudia Yesu, anajaza wakristo, anazaa matunda za Roho, anaongoza wakristo katika kweli, anasaidia na kuongoza mkristo, anaongoza mkristo katika maabudu, anaita watu na anawatuma katika kazi, anagawa karama kwa wakristo kwa ajili ya huduma mbalimbali kanisani (Mwanzo 1 : 2 ; Yohana 16 : 8 ; Matendo 5 : 3-‘ ; 3 : 5 ; Waroma 8 : 11 ; 14 :17 ; 15 :13 1 Wakorinto 12 : 4-6 ; 1 Wakorinto 12 : 13 ; Wagalatia 5 : 22-23 ; WWaefeso 1 : 13 ;3 :16-19 ; Tito 3 : 5 ; 1Yahana 2 : 20 na 27 ; Ufunuo 22 : 17-30).

Maulizo :

- Nini Biblia inatufunza kuhusu Mungu ?
- Mungu ni nani ?
- Taja nafsi tatu za Mungu
- Tofauti gani iliyo kati ya Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu ?
- Taja kazi za Roho Mtakatifu ndani ya mkristo.

2.3. Imani kuhusu uhumbaji

Toka kitabu cha Mwanzo hadi cha Ufunuo, Biblia inafundisha kwamba Mbingu, nchi na vyote vilivyomo viliumbwa na Mungu kwa Neno lake bila kutumia kitu iwayo chochote isipokuwa kwa kuhumba mwanadamu, nyama za pori na ndege ndio alitumia udongo (Mwanzo 2: 1-3; 2: 7; 2:19; 20: 11; Nehemia 9: 6; Zaburi 33: 6-9; 148: 1-6).

Maulizo:

- Vitu vilivyo mbingu na duniani vilitoka wapi?
- Taja tofauti iliyoko katika uhumbaji ya vitu na ya mwanadamu ?

2.4. Imani kuhusu Malaika

Biblia inafundisha kama Malaika ni roho walioumbwa na Mungu mbele ya kuumbwa kwa wanadamu. Malaika hawana mwili, awaweze kufa na kazi yao ni kumuabudu na kumusifu Mungu. Hawakubali kuabudiwa na wanadamu.
Shetani na mizimu ni malaika waliokosa mbinguni na kutupwa duniani kwa kuchunga ukumu ya mwisho (Mwanzo 2: 1; Yobu 38:4-7; Danieli 10: 13-21; Matayo 18: 10; 25: 41; 26:53; Luka 2:13; 20: 32-34; Wakolosai 2: 18; Waebrania 1: 7; 1 Pierre 3: 22; Yuda 6; Ufunuo 5: 11; 12: 7; 19: 10; 22: 8-9).

Maulizo:

- Malaika ni wanani?
- Sema tofauti kati ya Malaika na Shetani
- Je Mkristo anaruhusiwa kuabudu malaika ?

2.5. Imani kuhusu zambi

Biblia inafundisha ya kwamba Zambi ni matendo, masemi na mawazo yasioambatana na mapenzi ya Mungu.
Zambi ilianza katika shamba la Edeni wakati Adamu na Awa walikula tunda la mti wa kujua mema na mabaya (Mwanzo 3).

Zambi inajionyesha katika matunda yake inayotajwa katika Wagalatia 5: 19-20.
Mungu anachukia zambi ndio sababu anahitaji tuwe watu wenye ku kiri zambi zetu akituharifu kuhusu hasara ya zambi ambazo ni: kutengwa na Mungu, kuchukiza watu wengine, kifo na gazabu ya milele (Yohana 3:16).

Maulizo:

- Zambi ni nini na ilianza namna gani?
- Namna gani Mungu anatazama zambi ?
- Taja matunda ya Zambi
- Zambi ina hasara gani ?

2.6. Imani kuhusu Wokovu

Biblia inafundisha ya kwamba tumeokolea kwa Neema kwa njia ya Imani katika Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yetu.
Mungu alipoona ya kwamba zambi za wanadamu ni nyingi, alituma Yesu ulimwenguni ili awaokowe kupitia kifo chake msalabani.
Kumuamini Yesu ni kukiri zambi zetu na kumukubali kama Bwana na Mwokozi wa maisha yetu.
Kukiri zambi ni kujitambua mwenye zambi, kuzijuta, kuomba msamaa na kuamua kutokuzifanya tena.
Kwa hivi, Biblia inaonyesha kwamba hakuna hukumu tena kwa yeyoye anayekua ndani ya Yasu.
Wokovu ni jambo la muhimu na unasamani kubwa sababu Biblia inaonyesha kwamba mwenye zambi mmja akiokoka mbinguni kuna karamu kubwa (Luka 15 : 10, Matendo ya Mitume 4 : 12 ; 16 :31 ; Waroma 10 : 9).

Maulizo :

- Namna gani wanadamu wanaokolewa ?
- Kukiri zambi ina maana gani ?
- Faida gani tumepata katika kumwamini Yesu ?

2.7. Imani kuhusu Kanisa

Jina kanisa linatoka kwanye luga la Kigriki na linamaanisha *Walio itwa toka.* Ndio sababu, anisa ni umoja wa Watu walio itwa na Mungu toka ulimwengu ili wa mtumikie.
Katika Biblia Kanisa lina itwa *mwili wa Kristo, jamaa la watakatifu, zizi ambalo Kristo ndie mchungaji, Jengo linalo jengwa na mawe ambazo Yesu ndie jiwe la pembe, mchumba wa Kristo, bibi harusi wa Bwana.*
Kazi ya Kanisa na la wakristo katika dunia ni kutangaza Habari njema ya Kristo na kuleta watu wote wamkubali Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yao (Matayo 28 :19). Ndio sababu wakristo wanaitajika kuwa na mwenendo na ushuhuda mzuri kama nuru na chunvi ya dunia (Matayo 8 : 11 ; 10 : 7 ; 16 : 13-19 ; Yohana 17 :14-26 ; 20 : 21-23 ; Matendo 1 : 7-8 ; 2 : 32-47 ; 6 : 1-2 ; 13 : 1 ; Waroma 2 : 28-29 ; 4 : 16 ; 1 Wakorinto 3 : 5-9 ; 7 : 7 ; 11 : 1-17 ; 12 :3-33 ; 2 Wakorinto 5 : 11 ; 6 : 1Watesalonika 4 : 1-12 ; Ufunuo 5 : 9-10).

Maulizo :

- -Kanisa ni nini ?
- -Majina gani kanisa linatajwa nazo katika Biblia ?
- Kazi ya kanisa na la wakristo katika dunia ni gani ?

2.8. Imani kuhusu Sakramenta

Zehebu la 8ème CEPAC linatumia sakramenti mbili : ubatizo na meza ya Bwana.

Meza ya bwana ilihamuriwa na Yesu mwenyewe katika Matayo 26 : 26-29.
Ni wakristo walio batizwa kwa maji mengi tu ndio wanaruhusiwa kushiriki meza ya Bwana sababu ni wenye kuamini na kubatizwa tu ndio wanaruhusiwa kushiriki Meza ya Bwana (Matayo 26 :26-29 ; Marko 14 : 22-25 ; Luka 22 : 17-20 ; Yohana 6 : 28-58 ; 1 Wakorinto 10 : 14-21 ; 11 : 23-32).
Nilazima kwa wakristo kujitakasa na kutengeneza maisha yao mbele ya kushiriki Meza ya Bwana (1 Wakorinto 11 : 23-32).

Ubatizo ni sakramenti hamuriwa na Yesu pia (Matayo 28 : 19). Kwa hivyo, ubatizo ni sakamenta inayo shuhudia mbele ya Mungu na wanadamu ya kwamba tumemkubali Yesu Kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yetu.

Katika zehebu la 8ème CEPAC, ni ubatizo wa maji mengi ndio unaruhusiwa kufuatana na mfano wa ubatizo wa Kristo katika Yordani.
Ubatizo sio njia ya wokovu sababu haina uwezo wowote wa kuondoa zambi ; kwa hivyo, inashudia hazarani kwamba anaye batizwa amemuamini Yesu na amekufa na kufufuka pamoja na Kristo ili aishi maisha mapya. Kuona kwamba ubatizo imepewa kwa walio muamini Yesu Kristo, 8ème CEPAC haikubali ubatizo wa watoto wadogo wala ubatizo wa wafu sababu kiisha kifo hakuna wokovu tena.

Maulizo :

- Kuna aina ngapi za Sakramenti katika kanisa?
- Nani anastahili kushiriki meza ya Bwana ?
- Ubatizo ina maana gani ?
- Sababu gani ni ya maana kwa kila mkristo kubatizwa ?

2.9. Imani kuhusu siku za mwisho

Biblia inafundisha kwamba siku moja dunia itakwisha na Yesu atakuja kuchukuwa Kanisa na kwenda nalo mbinguni. Ndio sababu wakristo wanaitajika kuwa tayari siku zote sababu siku wala saa za kurudi kwa Yesu hazijulikane (Matayo 24:44; Luka 21:28; Matendo 1:11; 2:20; Wafilipi 1:16; 1Watesalonika 4: 13; 5: 2; 2 Watesalonika 1:1-2).

Biblia inafundisha ya kwamba mwisho wa dunia watu wote walio kufa watafufuliwa: Wakristo kwa raha ya milele pamoja na Kristo mbinguni na Wapagani kwa taabu ya moto wa milele pamoja na shetani. Kila mmoja akilipwa sawasawa na matendo yake hapa duniani (Danieli 12:2; Matayo 25: 13-46; Luka 19: 17-19; 1Wakorinto 6: 2-3; 2 Wakorinto 3: 10; Ufunuo 20: 6).

Maulizo:

- Biblia inafundisha nini kuhusu dunia na vitu viliovyomo?
- Tofauti gani itakayo kuwa kati ya wakristo na wapagani mwisho wa dunia ?
- Kwa nini wakristo wanaitajika kuwa tayari kila siku kwa kumlaki Yesu hewani ?

III. NJIA ZA KUKOMAA KIROHO

Kufananisha wokovu na kuzaliwa mara ya pili inaonyesha ya kwamba ni lazima kwa kila mkristo mpya kuelewa faida na umuimu wa kukomaa kiroho. Si lazima kwake kuendelea kuwa mkristo mchanga kila siku; lakini imamubidi kukomaa kiroho na kuwa mkristo mzima (spirituellement mûr).

Kwa mkristo mpya kukomaa kiroho kuna kanuni sita ambazo zinaweza kumsaidia.

3.1. Kufuata mafundisho

Kwa kukomaa kiroho ni lazima kwa mkristo mpya kushiriki na kufuata mafundisho. Haitoshi kwake kufuata mahubiri tu lakini mafundisho vilevile ni ya lazima kwake sababu inamusaidia kuelewa ile anayo amini. Mara nyingi wakristo wapya wanavutwa na walimu wa uongo ao na dini zingine zisizo faa sababu yakukosa kuelewa maandiko matakatifu.

Kwa kuhepuka hasara hii, kanisa linapashwa kuwa na mpango wa mafundisho kila juma. Hatari ni kwamba, baada ya kubatizwa wakristo wapya (hata wale wa zamani) hawafike tena kwa mafundisho na wanabaki wakristo wa juma pili (siku ya Mungu). Ni lazima wakristo wapewe mafundisho itakayo wasaidia kuelewa doctrine, mwenendo na mambo kazalika inayo weza kuwaletea shida ikiwa hawakuyaelewa.

Ni lazima pia mkristo mpya ashiriki mafundisho haya ambayo yatamusaidia kusimama imara, kuchunga na kuelewa imani yake na kutofautisha mafundisho ya uongo na ya kweli.

Katika barua yake ya pili kwa Timoteo, Mtume Paulo anamuonyesha mafaa ya neno la Mungu na matumizi yake : *Kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu, linafaa kwa kufundisha, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki, ili mutu wa Mungu awe mukamilifu, ametengenezwa kabisa katika kila tendo njema* (2 Timoteo 3: 16 – 17).
Katika andiko hili, Paulo anapenda kuharifu Timoteo ya kwamba ni vigumu kwa mkristo kukamilika bila mafundisho toka neno la Mungu. Nikusema, kila fundisho lisilotoka katika neno la Mungu (Biblia) na ambalo halijenge kanisa la Bwana halipashwe kuaminiwa na kushikwa.

Bila kushiriki mafundisho ni vigumu kwa mkristo mpya kukamilika na kukomaa kiroho.

3.2. Kufuata Mahubiri

Ikiwa mafundisho inasaidia mkristo kuelewa nini ana hamini, Mahubiri inamsaidia katika kumujenga kiroho (édification spirituelle).

Kila siku ya ibada, mkristo anapashwa kupata neno mpya toka mahubiri ambalo linamuhimiza katika safari yake ya kwenda mbingu. Hii inamaanisha kwamba kila mkristo anawajibika kushiriki kwa ibada na kufuata mahubiri ikiwa anapenda kukomaa kiroho.

Katika Waroma 16: 25, Mtume Paulo anaonyesha wazi namna gani mahubiri inahimarisha mkristo na namna gani mahubiri yake hayakuwa kwa maneno ya akili ya kuwashawishi watu, lakini katika Isahra za Roho na za nguvu (1 Wakorinto 2: 4). Nikusema, wakristo wanaitajika kujitahazari na mahubiri yasiyo toka

katika neno la Mungu ao yanayo toka watu wa kujipendeza na ambayo hayafae kwa kuwasaidia kukomaa kiroho.

Bila kushiriki kwa mahubiri ni vigumu kwa mkristo mpya kukamilika ao kukomaa kiroho.

3.3. Kusoma neno la Mungu kila siku

Kusoma neno la Mungu kila siku litamsaidia pia mkristo mpya kukomaa kiroho. Ndio sababu wakristo wanawajibika kuwa kila mmoja na Biblia yake nyumbani na mahali pote. Ni vigumu kwa mkristo kutii Neno la Mungu asipokuwa na muda wa kulisoma na kulicheuwa.
Ni lazima kwa kila mukristo kuwa na muda wa kusoma Neno la Mungu katika hali ya maombi akijiuliza *Nini Bwana anapenda kunifunza kupitia neno hili ninalotoka kusoma ?*

Kanisa la Beroya linakuwa mfano muzuri wa kuiga ikiwa mkristo mpya anapenda kukomaa kiroho na kuhepuka kudanganywa na walimu wa uwongo. Biblia inaonyesha ya kwamba *Watu hawa walikuwa wema kuliko wale wa Tesalonika, kwa sababu walipokea Neno kwa nia iliokuwa tayari kabisa, wakatafuta Maandiko kila siku kujua hakika ya maneno yale* (Matendo ya Mitume 17 : 11).

3.4. Kua na mda binafsi wa maombi

Kwa kukomaa kiroho mkristo mpya anaitaji kuwa na mupango binafsi wa maombi. Ni lazima awe na muda wa kuzungumuza na Mungu kila sika. Bila hivi atakuwa mkristo anaye kauka na muzaifu.
Haiwezekane kwa mkristo kuwa na nguvu za Mungu ikiwa hana muda wa maombi peke yake. Hii haimaanishe kwamba si lazima kushiriki kwa maombi na wengine, lakini anaitajika kuwa na mda wa kukutana na Bwana wake wao wawili.
Maombi ya binafsi inafaida nyingi kwa mkristo :

- Inamfunulia siri za Bwana
- Inampatia nguvu ya kushinda majaribu
- Inamsaidia kujitakasa
- Inamsadia kufahamu mapenzi ya Mungu katika maisha yake
- Inamsaidia kupata baraka za Mungu kiroho na kimwili.
- Inachochea karama

Bila maombi binafsi, si rahisi kwa mkristo kukomaa kiroho.

3.5. Kuomba mashauri

Ni lazima pia kwa mkristo kuwa tayari kuomba mashauri na kuyashika ikiwa yanaweza kujenga kanisa la Bwana. Ndio sababu kanisa linakuwa na mchungaji na wazee ili wapate kusaidia wakristo kwa mashauri wanaokua wachanga ao wanaokua na shida.

Biblia inaonyesha mengi kuusu hatari ya kukataa mashauri kwa maisha ya mwanadamu: *Yeye anayeonywa mara nyingi na anafanya shingo yake ngumu anavunjika gafula, pasipo njia ya kupona* (Mezali 29:1). Ni azima kwa mukristo kuomba mashauri ikiwa anatamani kukomaa kiroho.

3.6. Kushirikiana na wakristo wengine

Kama kiungo cha mwili ulio Kanisa, mkristo mpya anaitaji kushirikiana na wakristo wengine ili kupitia karama zao, wapate kumujenga na kumusaidia kukomaa kiroho.
Mtume Paulo anaonyesha faida ya karama mbalimbali katika kanisa (1 Wakorinto 12): nikusaidia kila mukristo kuleta muchango wake kwa maendeleo ya kazi ya Mungu wakijengana wao kwa wao. Waefeso 4: 11- 16 inahakikisha neno hili kwa kuonyesha kwamba huduma mbalimbali zinafaa kwa kusaidia wakristo wasiwe tena watoto wanaotupwa huku na huku na kuchukuliwa kwa kila upepo wa elimu , kwa hila ya watu, kwa ujanja, kwa udanganyifu mubaya bali waseme kweli katika mapendo.

KWA MWISHO

Sio raisi kuandika katika kitabu mafundisho ambayo mtu anayemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake anapashwa pokea.
Shida hiyi inatokana na kwamba ni Roho Mtakatifu peke yake ndie mwalimu mkubwa anayefahamu mafudisho gani inafaa kwa kila mtu.

Kitabu hiki ni msaada kwa wale wanao husika na shule la ubatizo katika makanisa ya CEPAC.
Pamoja na maandiko haya, mwalimu wa shule la ubatizo anawajibika kuwa mtu aliyekutana binafsi na Yesu, mtu wa maombi, anayesoma Neno la Mungu kila siku na anayekua na uhusiano mzuri na Mungu.
Basi, kwa yeye anaye tuita kumutumikiya na anaye tupatiya uwezo wa kumtumikiya ziwe sifa utukufu milee na milele, Amina.